

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TANO**

**KIKAO CHA SABA**

**10 NOVEMBA, 2021**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA TANO

**KIKAO CHA SABA – TAREHE 10 NOVEMBA, 2021**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tatu wa Bunge na Mkutano wa Nne wa Bunge pamoja na Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**69. MHESHIMIWA VENANT DAUD PROTAS (IGALULA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-


Je, ni lini Serikali itatekeleza agizo la Rais wa Awamu ya Tatu la kuitambua Kizengi kuwa Tarafa.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**70. MHESHIMIWA MUHARAMI SHABANI MKENGE (BAGAMOYO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuvisaidia vikundi vya BMU ili kuendeleza kasi ya upandaji Mikoko na kusafisha fukwe kuanzia Pwani ya Bagamoyo, Pangani hadi Tanga.



**WIZARA YA MADINI:**

**71. MHESHIMIWA HAMIS MOHAMED MWINJUMA (MUHEZA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, ni lini Serikali itawaruhusu Wachimbaji wadogo katika Kijiji cha Sakale Kata ya Mbomele


Wilayani Muheza kuanza uchimbaji wa Madini ya Dhahabu yaliyothibitishwa kupatikana katika Kijiji hicho.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**72. MHESHIMIWA AGNES ELIAS HOKORORO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutafuta teknolojia mbadala ili kunusuru afya za Wananchi wanaotumia zebaki kwa matumizi mbalimbali.



**73. MHESHIMIWA HALIMA JAMES MDEE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

(a) Je, tangu janga la CORONA lianze ni Watanzania wangapi wamepata maambukizi, wangapi wamekufa na wangapi wamepona;



(b) Je, ni fedha kiasi gani zimetengwa na Serikali na zimefanya nini na wapi katika kukabiliana na janga hili;

(c) Je, nini kinapelekea gharama za kupima COVID-19 kuwa kubwa na ni dawa gani zilizofanyiwa uchunguzi na kuthibitishwa kuwa zina uwezo wa kuzuia au kutibu COVID-19.

**WIZARA YA KILIMO:**

**74. MHESHIMIWA EDWIN ENOSY SWALLE  
(LUPEMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha zao la Chai nchini.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**75. MHESHIMIWA FRANCIS KUMBA NDULANE  
(KILWA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, ni lini Serikali itajenga Masoko ya kisasa ya kuuzia Samaki hasa katika Kata za Somanga na Kivinje ambazo upatikanaji wa Samaki ni mkubwa ili kuboresha maisha ya Wavuvi na Wilaya ya Kilwa kiuchumi.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**76. MHESHIMIWA STANLAUS HAROON NYONGO (MASWA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kalandoto hadi Meatu.

**77. MHESHIMIWA EMMANUEL MAGENI KASALALI (SUMVE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini barabara ya kutoka Magu – Bukwimba hadi Ngudu itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami ili kuunganisha makao makuu ya

Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba na makao makuu ya Mkoa wa Mwanza.

**78. MHESHIMIWA SEBASTIAN SIMON KAPUFI (MPANDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini tatizo la upungufu wa Mabehewa ya abiria na mizigo litatatuliwa katika Kituo cha Mpanda.

**IV. HOJA ZA KAMATI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tatu wa Bunge na Mkutano wa Nne wa Bunge pamoja na Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009.

**DODOMA  
10 NOVEMBA, 2021**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**